King County

Ofisi ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria (OLEO)

Machi 20, 2023

KWA: Patti Cole-Tindall, Liwali, Ofisi ya Sheriff ya Kaunti ya King (Ofisi ya Sheriff)

NAKILI: Jesse Anderson, Naibu wa Liwali, Ofisi ya Liwali
Jonathan Hoffman, Meneja wa Viwango vya Kitaaluma(Professional Standards Manager), Ofisi ya Liwali
Karan Gill, Naibu Mkuu wa Wafanyakazi(Deputy Chief of Staff), Ofisi ya Mtendaji wa Kaunti ya King (King County Executive Office, KCEO)
Anita Whitfield, Afisa Mkuu wa Usawa na Ujumuishaji, KCEO

KUTOKA: Tamer Abouzeid, Mkurugenzi, Ofisi ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria (Office of Law Enforcement Oversight,OLEO)

KUHUSU: Kutumia Wakalimani, Mwongozo wa Maagizo ya Jumla (General Orders Manual, GOM) 16.04.000 na GOM 6.00.000

Kufuatia Uchunguzi wa Ndani nambari IIU2022-175, OLEO imepitia GOM 16.04.000 ya Ofisi ya Liwali kuhusu Kutumia Wakalimani. Kama ilivyoainishwa katika barua ya OLEO katika Kitengo cha Uchunguzi wa Ndani mnamo Novemba 30, 2022, GOM 16.04.000 inashughulikia mahitaji fulani ya wakati na jinsi ya kutumia wakalimani, lakini kwa kiasi kikubwa inahusu tu tafsiri ya lugha ya ishara kwa watu wenye ulemavu wa kusikia na haishughuliki itifaki za mawasiliano na watu wenye Umilisi Mdogo wa Lugha ya Kiingereza (Limited-English Proficiency, LEP) kikamilifu.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa GOM 6.00.000 kuhusu Matumizi ya Nguvu, maafisa wa polisi wanatakiwa kuzingatia vizuizi vya lugha wanapofanya uamuzi wa kutumia na kudhibiti nguvu. Hata hivyo, sera hiyo haina maelezo ya kutosha kuhusu rasilimali za upatikanaji wa lugha au itifaki za kuripoti vizuizi vya lugha na matumizi ya nguvu.

Kwa uwazi na uthabiti, Ofisi ya Liwali inapaswa kuendeleza na kupitisha sera ya upatikanaji wa lugha inayoendana na miongozo ya serikali kuu (federal guidelines), Sheria ya Kaunti ya King Kodi ya Kaunti ya King, (King County Code, KCC §2.15.030), mahitaji ya Upatikanaji wa Lugha na Mawasiliano ya Kaunti, na taratibu bora za kitaifa. **Kumbukumbu hii inaeleza mapendekezo ya kurekebisha sera ya Ofisi ya Liwali katika Sura ya 16 na 6 ya GOM ili kuboresha upatikanaji wa lugha kwa LEP**

Katika maandalizi ya kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya sera, OLEO ilipitia sera za upatikanaji wa lugha katika sekta za mamlaka sawia pamoja na utafiti wa mbinu bora kutoka kwa Idara ya Haki,[i] Chama cha Kimataifa cha Wakuu wa Polisi (International Association of Chiefs of Police),[ii] na Taasisi ya Vera ya Haki (Vera Institute for Justice).[iii]

Kwa lengo la kuhakikisha mawasiliano kwa wakati na kwa usahihi na upatikanaji wa lugha kwa huduma za Ofisi ya Liwali kwa watu wote bila kujali lugha ya msingi,[iv] asili ya kitaifa, au ulemavu, OLEO inatoa mapendekezo yafuatayo:

PENDEKEZO LA 1.

Iweke wazi kuwa huduma za ukalimani zitatolewa wakati wowote wa shughuli za utekelezaji wa sheria kwa mtu mwenye ulemavu wa kusikia au mtu mwenye Umilisi Mdogo wa Lugha ya Kiingereza (LEP).

Kwa sasa – na kulingana na Kanuni ya Sheria Iliyorekebishwa ya Washington RCW 2.43.120 – GOM 16.04.000 ina bainisha wakati ambapo mkalimani wa lugha ya ishara anapaswa kuitwa, yaani, kwa watu wenye ulemavu wa kusikia. Sera hii haitoi mwongozo sawa kuhusu LEP.

Mapendekezo ya OLEO ni kwamba mkalimani aitwe kwa shughuli yoyote ya utekelezaji wa sheria kwa mtu mwenye ulemavu wa kusikia au wenye LEP ila pale ambapo mtu mwenyewe ataomba vinginevyo,[v] na kwa mahojiano yoyote na mtoto mdogo ambaye mzazi, mlezi, au mtunzi wake ni mlemavu wa kusikia au mwenye LEP. Katika tukio la kukamatwa kwa watu wenye ulemavu wa kusikia au wenye LEP, mahojiano yote yanapaswa kuahirishwa hadi mkalimani atakapopatikana.

Mapendekezo haya yanaondoa kizuizi cha kumwita mkalimani tu katika maingiliano yanayohusiana na uchunguzi wa jinai na kuyalinganisha sera za Ofisi ya Liwali na miongozo ya serikali kuu na Sheria ya Kaunti ya King inayohitaji upatikanaji wa lugha sawa kwa huduma zote.[vi] Aidha, kulingana na sekta za mamlaka sawia, OLEO inapendekeza kwamba wakati Ofisi ya Liwali inatumwa kwenye tukio linalohusisha mtu mwenye mlemavu wa kusikia au mwenye LEP, huduma za tafsiri (interpretation services) zitolewe mahali pa tukio.[vii] Ofisi ya Liwali inapaswa kushirikiana na Ofisi ya Usawa ya Kaunti, Haki ya Kijamii na Rangi ya Kaunti (County Office of Equity, Racial and Social Justice) kuanzisha itifaki ya kuwatuma wakalimani wa ana kwa ana waliohitimu.[viii]

PENDEKEZO LA 2.

Kuweka wazi kwamba wakalimani wataitwa katika shughuli za utekelezaji wa sheria bila kujali hali ya mtu kama mwathirika, shahidi, au mtuhumiwa.

Sera ya sasa katika Sura ya 16 inasema kwamba mkalimani wa lugha ya ishara ataitwa kwa ajili ya mwathirika au shahidi ambaye ni mlemavu wa kusikia. Hata hivyo, sheria ya serikali inasema wazi kwamba mkalimani ataitwa iwe mtu ni mwathirika, shahidi, au mtuhumiwa[ix].

PENDEKEZO LA 3.

Kuratibu huduma za ziada za ukalimani kwa watu wenye LEP zaidi ya AT&T Language Line.

Sera ya sasa katika Sura ya 16 haitoi itifaki ya kufasiriwa na wakalimani wa ana kwa ana waliohitimu au manaibu wa liwali wanaozungumza lugha mbili.[x] OLEO inapendekeza (a) matumizi ya wakalimani waliohitimu, ikiwa ni pamoja na maafisa wa Ofisi ya Liwali wanaozungumza lugha mbili wa Ofisi ya Liwali, ambao wameidhinishwa na wana mafunzo maalum ya kutafsiri katika muktadha wa sheria ya jinai, na (b) kwamba wakalimani wa ana kwa ana wapewe kipaumbele kuliko wakalimani wa simu.[xi]

OLEO inapendekeza kwamba wakalimani wa ana kwa ana waliothibitishwa *watatumiwa* mtu atakapo kukamatwa. Ikiwa mkalimani wa ana kwa ana amaepigiwa na hapatikani, wanachama wanapaswa kunakili taarifa hiyo na kutumia mkalimani wa simu kama vile huduma ya Langauge line. Ufasiri uliohitimu unapaswa kuwa wa lazima kwa taarifa za haki za kikatiba, mahojiano, au kuandika taarifa. Taratibu bora ni kutafsiri na kutoa nakala zilizoandikwa za onyo la Miranda kwa watu wenye ulemavu wa kusikia au wenye LEP katika lugha yao ya msingi ili kuhakikisha usahihi.[xii] Mkalimani anapaswa awe ikiwa mtu huyo hawezi kusoma au ana maswali kuhusu haki zake.

Zaidi ya hayo, OLEO inapendekeza kujumuishwa kwa ushauri wa tafsiri ya ziada pamoja na onyo[xiii] la Miranda kama lugha ifuatayo:

> "Ikiwa una ulemavu wa kusikia au Kiingereza si lugha yako ya msingi, Ofisi ya Sheriff ya Kaunti ya King ina wajibu wa kukupa mkalimani bila malipo na itaahirisha mahojiano hadi mkalimani atakapowasili."

PENDEKEZO LA 4.

Ongeza vikwazo vya ni nani asiyepaswa kuwa mkalimani na zijumuishe shughuli za utekelezaji wa sheria zinazohusisha watu wenye LEP.

GOM 16.04.025 kwa sasa inaelekeza maafisa wasitumie marafiki au wanafamilia kutafsiri lugha ya ishara. Kwa uthabiti, aina hii ya kizuizi inapaswa kutumika kwa aina zote za ukalimani, si kwa lugha ya ishara tu.

Zaidi ya hayo, OLEO inapendekeza kuwa vizuizi hivi viongezwe ili kutohusisha marafiki, wanafamilia, wajitoleaji, wapita njia, au watoto kwenye ukalimani katika shughuli yoyote ya utekelezaji wa sheria isipokuwa kuna sababu ya usalama inayohitaji mawasiliano ya haraka. Mazungumzo yoyote yanayohusisha mkalimani asiyehitimu yanapaswa kurekodiwa kwa kamera halisi au kifaa cha kurekodi sauti (ikiwa mtu wa tatu au mtu mwenye LEP anakataa kurekodiwa, kukataa huko kunapaswa kurekodiwa). Taarifa yoyote inayotolewa na mkalimani asiyehitimu inapaswa kuthibitishwa na mkalimani aliyehitimu mapema iwezekanavyo. Mwongozo wa ziada wa kuripoti unapaswa kutumika ili kunakili asili ya hali yoyote ya dharura na matumizi ya wakalimani wasiohitimu.

PENDEKEZO LA 5.

Ongeza sera na utaratibu wa kubaini lugha ya msingi ya mtu.

Kwa sasa hakuna itifaki iliyoainishwa kusaidia maafisa kubaini lugha ya msingi ya mtu. Mamlaka kadhaa zinazofanana hutoa kadi za "I Speak" kwa maafisa, ambazo Ofisi ya Usawa ya Kaunti, Haki ya Kijamii na Rangi ya Kaunti tayari imeandaa kwa lugha 36 zinazozungumzwa zaidi katika Kaunti.[xiv] Ofisi ya Liwali inapaswa kushirikiana na Programu ya Upatikanaji wa Lugha ya Kaunti (County Language Access Program)[xv] kubadili rasilimali hii kwa matumizi ya 'maafisa' na kueleza taratibu za kubaini lugha ya msingi katika GOM 16.04.000.

PENDEKEZO LA 6.

Ongeza lugha ya matumizi ya vifaa mbadala vya msaada na mashine ya uchapaji ya mawasiliano.

Kama ilivyoandikwa, GOM 16.04.000 haijatoa miongozo kuhusu matumizi ya vifaa mbadala vya msaada.[xvi] Miongozo ya serikali kuu inahitaji kwamba ombi la mtu mlemavu la usaidizi mbadala liheshimiwe, isipokuwa kama kuna njia nyingine nzuri ya mawasiliano.[xvii]

OLEO inapendekeza kuongeza lugha ili kufafanua kuwa ombi la vifaa mbadala vya msaada linapaswa kuheshimiwa. Maombi yote kama hayo yanapaswa kunakiliwa katika ripoti ya naibu wa liwali. OLEO pia inapendekeza kwamba ikiwa mwanachama atakataa ombi la mtu mwenye ulemavu wa kusikia la kifaa mbadala cha msaada ili kuwasiliana, mwanachama anapaswa kunakili na kutoa sababu za kukataa katika ripoti yao.

Aidha, ili kuhakikisha upatikanaji sawa wa huduma, sera inapaswa kubainisha kwamba watu wenye ulemavu wa kusikia watawezeshwa kufikia Mashine ya Uchapaji ya Mawasiliano (TTY, pia inajulikana kama kifaa cha mawasiliano kwa watu wenye ulemavu wa kusikia, au TDD) ili kupiga simu katika hali yoyote ambapo mtu asiye na ulemavu wa kusikia angetumia simu. Wanachama pia wanapaswa kukubali simu zinazopigwa na watu wenye ulemavu wa kusikia kupitia Huduma ya Uunganisho wa Mawasiliano (Telecommunications Relay Service).[xviii]

PENDEKEZO LA 7.

Kuweka mahitaji ya ziada ya kuripoti ili kunakili ulemavu wa kusikia au vikwazo vya lugha.

Huku GOM 16.04.030 ikihitaji maafisa kuripoti utumizi wa mkalimani wa lugha ya ishara, OLEO inapendekeza maelekezo ya kuripoti yafanyiwe upanuzi kujumuisha unakili wa:

- uwepo wa ulemavu wa kusikia au vikwazo vya lugha;
- maombi ya na kutumia au kukataliwa kwa vifaa vya msaada;
- njia ambayo maafisa walitumia kutambua lugha ya msingi ya mtu;
- kutumia wakalimani wa simu kama vile kupitia huduma ya language line;

- kutumia wakalimani waliohitimu; na
- kutumia marafiki, familia, wajitoleaji, wapita njia,, au watoto waliotumika kama wakalimani na uhusiano wao na mtuhumiwa.

PENDEKEZO LA 8.

Kubadilisha utoaji wa onyo kabla ya kutumia nguvu ili kuagiza maafisa kufikiria uwezekano wa ulemavu wa kusikia au vikwazo vya lugha vinavyoweza kuathiri ufahamu au utii.

GOM 6.00.000 tayari inawaagiza maafisa kujitambulisha, kutoa tahadhari za kinywa, na kutoa fursa ya kutosha kutii kabla ya kufyatua risasi au kutumia mbinu nyingine za nguvu. Kulingana na utaratibu wa mashirika sawia [xix]OLEO inapendekeza kujumuishwa kwa lugha ifuatayo:

> "Wanachama wanapaswa kuwa makini kwamba kunaweza kuwa na ulemavu wa kusikia au kizuizi cha lugha kinachozuia uelewa wa maagizo. Katika hali hizi, wanachama watajaribu kubaini njia zingine ambazo wanaweza kutumia kutoa onyo ikiwa inawezekana."

PENDEKEZO LA 9.

Hitaji la kuripoti uwepo wa sifa na hali zilizoorodheshwa na athari yake kwenye maamuzi muhimu kuhusu utumizi ya nguvu.

GOM 6.00.000 iliyochapishwa hivi karibuni kuhusu Matumizi ya Nguvu inahitaji maafisa kuzingatia sifa na hali kadhaa ikiwa ni pamoja na vikwazo vya lugha kabla ya kutumia nguvu.[xx]

Hata hivyo, GOM 6.01.000 kuhusu Uchunguzi/Ripoti ya Matumizi ya Nguvu na Matukio Makubwa haijaelekeza lini au jinsi ya kunakili sifa na hali hizi. OLEO inapendekeza kuwepo kwa mahitaji ya ziada ya kuripoti ili kunakili:

- uwepo wa mojawapo ya sifa na hali zilizoorodheshwa katika sera, hasa kwa mapitio haya ya sera, uwepo wa kizuizi cha lugha;
- tahadhari yoyote au maagizo yaliyotolewa; na
- ufahamu wa maagizo hayo.

---

[i] Idara ya Haki ya Marekani (U.S. Department of Justice), "Mwongozo wa Rasilimali za LEP kwa Utekelezaji wa Sheria," n.d., https://www.dhs.gov/sites/default/files/publications/lep-resouce-guide-law-enforcement 0.pdf.

[ii] Bharathi S. Venkatraman, "Kupotea katika Tafsiri: Idadi Ndogo ya Watu Wenye Umilisi Mdogo wa LughaKiingereza na Polisi," *Mkuu wa Polisi*, 73:4, 2006, Chama cha Kimataifa cha Wakuu wa Polisi, https://www.policechiefmagazine.org/lost-in-translation-limited-english-proficient-populations-and-the-police/?ref=b34840803136937f3b3e631e13395e51.

[iii] Susan Shah, Insha Rahman, na Anita Khashu, "Kushinda Vizuizi vya Lugha: Suluhu kwa Utekelezaji wa Sheria,"

Taasisi ya Vera ya Haki na Idara ya Haki ya Marekani Huduma za Polisi Zilizoelekezwa kwa Jamii, 2007, https://www.vera.org/publications/overcoming-language-barriers-solutions-for-law-enforcement na Susan Shah na Rodolfo Estrada, "Kuwezesha Uelewa wa Lugha: Mbinu Zinazofaulu kwa Utekelezaji wa Sheria," Taasisi ya Vera ya Haki, 2009, https://www.vera.org/publications/bridging-the-language-divide-promising-practices-for-law-enforcement.

[iv] "Lugha ya Msingi" ina maanisha lugha ambayo mtu anaweza kuitumia kuwasiliana kwa ufanisi. (Chanzo cha ufafanuzi: Agizo la Jumla la Idara ya Polisi ya San Francisco (San Francisco Police Department General Order) 5.20.)

[v] Tazama Pendekezo la 6 kwa majadiliano ya visaidizi mbadala.

[vi] Kwa muhtasari kamili wa mahitaji yanayotumika, tazama Mahitaji ya Upatikanaji wa Lugha na Mawasiliano ya Ofisi ya Usawa ya Kaunti na Haki za Jamii ya Kaunti ya King, https://kingcounty.gov/~/media/elected/executive/equity-social-justice/Immigrant-and-Refugee/LanguageAccessOrd/Language-Access-Requirements.ashx?la=en.

[vii] Tazama, kwa mfano, Mwongozo wa Idara ya Polisi ya Seattle (Seattle Police Department Manual)15.250.F.3. – Wakalimani na Watafsiri wa Lugha, https://www.seattle.gov/police-manual/title-15---primary-investigation/15250---interpreters-and-translators.

[viii] Tazama Pendekezo la 3 kwa majadiliano ya wakalimani wa ana kwa ana waliohitimu.

[ix] Tazama Kanuni ya Sheria Iliyorekebishwa ya Washington (Revised Code of Washington, RCW) 2.42.120.

[x] Sehemu pekee ya GOM 16.04.00 inayohusu kutumia Wakalimani husika kwa watu wenye LEP ni 16.04.035 inayoelezea itifaki ya kutumia AT&T Language Line.

[xi] Tazama, kwa mfano, Agizo la Jumla la Idara ya Polisi ya San Francisco 5.20 III (D), Huduma za Upatikanaji wa Lugha kwa Watu Wenye LEP, Agizo la Upendeleo https://www.sanfranciscopolice.org/sites/default/files/2018-11/DG05.20%20Language%20Access%20Services%20for%20Limited%20English%20Proficient%20%28LEP%29%20Persons.pdf.

[xii] Manuel Triano-López, "Hatua za kabla ya kesi za kukamatwa na mahojiano ya polisi: Athari kwa wakalimani na watafsiri nchini Marekani."

[xiii] Tazama, kwa mfano, Mwongozo wa Idara ya Polisi ya Seattle 6.150 –Kuwa shauri Watu kuhusu Haki ya kuwa na Wakili na Miranda (9) "Maafisa Wanapaswa Kujumuisha Onyo la Ziada kwa Watu Wenye Ulemavu wa Kusikia", https://www.seattle.gov/police-manual/title-6---arrests-search-and-seizure/6150---advising-persons-of-right-to-counsel-and-miranda.

[xiv] Tazama Kadi za "I Speak" za Kaunti ya King, https://kingcounty.gov/~/media/elected/executive/equity-social-justice/Immigrant-and-Refugee/LanguageAccessOrd/I_Speak_Cards_FINAL.ashx?la=en.

[xv] Tazama Programu ya Upatikanaji wa Lugha ya Kaunti ya King, (County Language Access Program)https://kingcounty.gov/audience/employees/translation-interpretation.aspx.

[xvi] Vifaa mbadala vya msaada ni zana zinazotumika kuwasiliana na watu wenye ulemavu au upungufu wa uwezo. Hii inaweza kujumuisha, lakini siyo tu, matumizi ya ishara au vifaa vya kuona; karatasi na kalamu au penseli kubadilishana maandishi; kompyuta au mashine ya uchapaji ya mawasiliano; mfumo au kifaa cha kusikiliza cha msaada ili kuongeza sauti; mashine ya uchapaji ya mawasiliano (TTY) au simu za video (huduma ya uhuamishaji wa video au VRS); maandishi yaliyorekodiwa; wasomi waliohitimu; au mkalimani aliyehitimu. (Chanzo cha ufafanuzi: Mwongozo wa Sera ya Idara ya Polisi ya Spokane (Spokane Police Department Policy Manual) 370.)

[xvii] Idara ya Haki za Binadamu ya Marekani, Sehemu ya Haki za Ulemavu, "Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Sheria ya Watu Wenye Ulemavu na Utekelezaji wa Sheria," 2020, https://archive.ada.gov/q&a law.htm.

[xviii] Tazama, kwa mfano, Mwongozo wa Maelekezo wa Idara ya Polisi ya Portland 06.40.36 Mawasiliano na Watu Wenye Ulemavu wa Kusikia na Watu Wenye Umilisi Mdogo wa Kiingereza, https://www.portlandoregon.gov/police/article/533213.

[xix] Tazama, kwa mfano, Mwongozo wa Maelekezo wa Idara ya Polisi ya Portland, 1010.00 Matumizi ya Nguvu 5.1.1 https://www.portland.gov/policies/police-directives/weapons-ammunition-equipment-1000/101000-use-force.

[xx] Sifa na hali hizi ni pamoja na: hali ya kimwili; ujauzito; umri; dalili za ulemavu wa kiakili, tabia, au kimwili; upungufu wa akili au ufanisi wa kijamii unaohusiana na matumizi ya dawa au pombe; mawazo ya kujiumiza; kizuizi cha lugha; au uwepo wa watoto.